KATIBA YA KICOBA

Mobi Saccos

Arusha

1. **JINA NA ANUANI**

- Jina la kikundi litakuwa **Mob Saccos**
- Anuani ya kikundi S.L.P
- Tarehe ya kuanzishwa 1/9/2020
- Idadi ya wananchama waanzilishi **20**
- Eneo la shughuli za kikundi litakuwa **Mobisol HQ - Arusha**
- Kikundi namba **1.**
- Fungamanisho (Common Bond) ni Wafanyakazi wa Mobisol

2. MADHUMUNI YA KIKUNDI

Madhumuni ya kikundi hiki ni

- Kuinua, kustawisha na kuboresha hali ya maisha ya wananchama
- Kupata mahali pa kuweka fedha za wanachama kwa usalama
- Kupata mikopo yenye masharti nafuu ndani ya kikundi ya kuendeshea Biashara na kuhudumia jamii
- Kuwekeza fedha ili kupata faida
- Kujenga utamaduni wa kununua Hisa, kujituma kukopa na kutumia vizuri mikopo.

3. MATARAJIO YA KIKUNDI ILI KUFIKIA MADHUMUNI

- Wanakikundi kununua Hisa
- Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wanachama
- Kuanzisha na kuendeleza shughuli yoyote ya ki-uchumi na kijamii kwa manufaa ya wanachama kama itavyo kubaliwa na wanachama wote wa kikundi
- Kujenga tabia ya kuweka akiba ndani ya kikundi kwa njia ya kununua Hisa kama utaratibu wa VICOBA unavyoeleza.
- Kutoa ushauri wa ki-uchumi, kifedha na kibiashara ili wanachama waweze kujenga tabia ya kuchukua mikopo yenye manufaa.
- Kujenga misingi imara ya kudhibiti ubadhilifu na wizi kwenye kikundi
- Kujenga utamaduni wa kulipa madeni kikamilifu

4. MAMLAKA YA KIKUNDI

- Kufanya kazi na kuchukua hatua yoyote kwa makusudi ya kutimiza madhumuni yaliyotajwa kwenye sheria hizi
- Kukopa, kukopesha na kudhibiti ulipaji wa mikopo kwa wanachama wasio lipa mikopo kwa wakati
- Kushitaki na kushitakiwa
- Kumiliki mali zinazo ondosheka na zisizo ondosheka

5. WAJIBU WA KIKUNDI

- Kutowabagua wanaotaka kujiunga na kikundi ila kwa kuzingatia idadi iliowekwa na kikundi ambayo ni jumla ya watu 30
- Kuweka mazingira bora kwa wanachama ya kununua hisa, mfuko wa jamii, kutoa faini na kukopa

- Kulinda maslahi ya wanachama
- Kutafuta wanachama wapya kwa kushirikiana na wanachama wengine.

6. UANACHAMA

Wanachama watakuwa :-

- Wanachama wote walio jiunga wakati wa uhamasishaji wa kikundi hiki na ambao wanaendelea kununua hisa katika kikundi
- Wanachama wapya watakao jiunga baada ya kutimiza masharti kjiunga na kikundi ikiwemo kuhudhuria mafunzo ya VICOBA na kushiriki kikamilifu kama utaratibu wa VICOBA unavyo eleza nahii itajitokeza kama kuna nafasi katika kikundi (wanachama wasipungue 15 na wasizidi 30)

7. SIFA ZA MWANACHAMA

- Awe mwenye umri usio pungua miaka kumi na nane
- Awe mwenye tabia nzuri mwaminifu na akili timamu
- Awe mwenye uwezo wa kununua hisa angalau mbili kila mwezi na mwenye uwezo wa kuhudhuria mikutano
- Awe tayari kufuata sheria na kanuni za kikundi hiki
- Awe mwenye uwezo wa kusimamia mradi wake kikamilifu.

8. TARATIBU ZA KUJIUNGA KATIKA KIKUNDI

- Maombi ya mwanachama yatafanyika kwa njia ya maandishi kwa mwenyekiti wa kikundi na mwenyekiti atawasilisha kwa wanachama wa kikundi na wakimkubali basi atataarifiwa kwa barua na kuelezwa hatua ambazo anatakiwa kuzifuata ili awe mwanachama kamili
- Ataandikishwa kwenye daftari/leja la kikundi

9. WAJIBU WA MWANACHAMA

- Kununua Hisa kama ilivyopangwa
- Kulipa madeni yote kikamilifu kwa muda uliopangwa
- Kuheshimu mikataba ikiwa ni pamoja na kulipa mkopo alio udhamini endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake kama alivyoahidi bila sababu za msingi. *Kuheshimu mkataba ikiwa pamoja na kukubali Hisa na dhamana alizoweka kuuzwa ili kufidia deni analodaiwa ndani ya kikundi*
- Kuwa mwaminifu ndani na nje ya kikundi

- Kubeba dhamana iwapo janga lolote litatokea dhidi ya hisa za wanachama
- Kutoa taarifa kwenye uongozi wa kikundi iwapo kiongozi anatoa huduma kwa upendeleo au anafanya jambo lolote linalo hatarisha maslahi ya kikundi
- Kuhudhuria vikao vyote vya kikundi vinavyo mhusu
- Kujielimisha kuhusu shughuli zote za kikundi
- Kuzingatia sheria za kikundi kikamilifu ikiwemo kulipa faini ndani ya kikundi kama inavyotakiwa bila kuonyesha ubishi au dharau kwa uongozi au kwa wanachama husika.

10. HAKI ZA MWANANCHAMA

- Kushiriki katika shughuli zote za kikundi kwa kufuata kanuni na taratibu za kikundi hiki
- Kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya kikundi
- Kuchagua au kuchaguliwa

11. KUTEUA MRITHI

- Kila mwanachama atamteua mrithi wake ambaye atakuwa na haki ya kulipwa hisa na mafao yote anayostahili (na hili litakuwa siri ndani ya kikundi)
- Mwanachama anayo haki ya kubadilisha jina la mirthi kila mwaka na kila uteuzi utaandikwa katika daftari la wanachama na mwanachama mwenyewe ataweka sahihi.

12. KUSIMAMISHWA UANACHAMA

- Mwanachama atasimamishwa kwa sababu ya kushindwa kulipa mkopo wake katika muda ulio pangwa na kikundi pasipo kuwa na sababu inayokubalika na wanachama wengine.
- Kufanya kitendo chochote ambacho kikundi kitaridhika kuwa ni kitendo cha kutokuwa mwaminifu na kinyume na maadili ya kikundi Mwanachama huyu atatozwa faini ya shilingi elfu tano mara ya pili atafukuzwa uanachama na 15% ya fedha zake zitakatwa kwa ajili ya usumbufu.
- Kuacha kuhudhuria katika mikutano ya kikundi mara nne mfululizo bila sababu maalumu na kutoshiriki kikamilifu kwenye shughuli za kikundi.

13. UANACHAMA UTAKOMA KWA

- Kuchukua hisa zake zote kwenye kikundi
- Ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari

- Kufukuzwa uanachama katika kikundi kwa kupigiwa kura isiyopungua theluthi mbili ya waliohudhuria nahii nia baada ya kupewa nafasi ya kujitetea kutokana na makosa aliyo yafanya.
- Kuandika barua ya kujitoa katika kikundi na atapewa mafao yake ndani ya siku tisini (90).

14. HISA

- Thamani ya hisa ni **shilingi 20,000** kiwango hiki kitakuwa kinabadilika kila mwaka kutokana na maendeleo ya wanachama wa kikundi
- Hisa ni mali ya mwanachama kwa hiyo hairuhusiwi kuchukua hisa za wanachama kununulia rasilimali za kikundi
- Mwanachama inabidi anunue hisa nyingi kwa faida yake mwenyewe
- Kila mwanachama anapaswa kuweka Hisa kupitia M-Koba, na Hisa zake zitaonekana katika akaunti ya kikundi kwa idadi ya hisa zake ambazo amekuwa akilipia.
- Faida ya kikundi itakayopatikana kutokana na mikopo itakayochukuliwa itagawanywa kwa wanachama kulingana na idadi ya hisa za wanachama. Mwanachama atakaye nunua hisa nyingi atakuwa na faida kubwa na atakayenunua hisa chache atapata faida ndogo.
- Iwapo mwanachama ana mkopo, hisa zake hazitaruhusiwa kuchukuliwa hadi amalize deni lake au la mwanachama aliye mdhamini ndani ya kikundi.
- Mwanachama ambaye hatanunua hisa katika kikundi atatakiwa kulipa faini ya shilingi 5,000.
- Kila mwanachama ataweza kufatilia kiwango cha hisa, mfuko wa jamii, mikopo na marejesho yake, kupitia EXCEL ambayo itatumwa kila baada ya kikao kufanyika.
- Fedha yote ya kikundi itahifadhiwa kwenye M-Koba, na mwanachama hatatakiwa kubaki na fedha, au kiongozi.

15. BIMA YA MKOPO YA KIKUNDI

Kila mwanachama atatakiwa kutoa 2% ya mkopo wake ili kuukinga mkopo wake dhidi ya janga la Kifo. Mfuko huu utakuwa na jukumu la kuhudumia janga litakalotokea baada ya mwanachama kukopa mkopo wa kuendeshea biasshara/mradi. Mwanachama akifariki deni lake litalipwa na bima ya kikundi na malimbikizo yatakabidhiwa kwa mrithi wake.

16. MFUKO WA ELIMU NA AFYA

Kila mwachama atatakiwa kuchangia shilingi 5,000 kwa mwezi kwa ajili ya mfuko wa Jamii. Mfuko huu utakopeshwa kwa wanachama kutokana na matatizo mbalimbali ya kijamii k.m. Afya, Elimu, Msiba, Harusi, kuibiwa vitu na nyumba kuungua. Mfuko huu utakopeshwa kwa muda wa **miezi mitatu/mwezi mmoja** na mkopaji atarudisha mkopo huo bila ziada/riba ya mkopo kwenye kikundi chake.

Mkopo huu utaruhusiwa kukopeshwa kwa ajili ya familia ya mkopaji

Mfuko huu ni mali ya wanachama na iwapo mwanachama atajiondoa katika kikundi hiki atajumlishiwa fedha zake na kupewa pamoja na mfuko wa Hisa.

17. HESABU ZA KIKUNDI

- Mwaka wa fedha wa kikundi utaanzia tarehe 1/9 hadi 1/9 kila mwaka
- Kikundi kitaandika vitabu vya hesabu na kutunza kumbukumbu muhimu
- Muhtasari wa mahesabu ya fedha za kikundi itatolewa kila mwezi.

18. KAMATI YA UTENDAJI

- Kamati ya Utendaji ya kikundi itakuwa na wajumbe watano kwa mujibu wa kanuni za vikundi vya VICOBA. Mwenyekiti, Katibu na Mweka hazina
- Wajumbe wa Kamati ya Utendaji watashika madaraka wa muda wa mwaka mmoja na wanaweza kugombea tena kama watakuwa tayari kufanya hivyo.
- Ni vyema kamati ya utendaji iwahamasishe wanachama kukopa fedha katika kikundi ili waweze kuboresha maisha yao. Ni vyema fedha zote zikopeshwe kwa wanachama badala ya kukaa benki (M-koba - TPB).
- Kamati ya Utendaji itakuwa na mamlaka ya kusimamia shughuli zote za kikundi zilizo amuliwa na wanachama wa kikundi.
- Kupokea maombi ya wanachama wanaotaka kujiunga
- Maombi ya wanachama yatajadiliwa na wanachama wote katika kikundi na mwanachama atakaye jiunga ni muhimu akawa kwenye kikundi kimoja na Yule aliye mleta.
- Kuhakikisha kuwa wakopaji wanarejesha madeni yao kama walivyoahidi na kuwachukulia hatua za kisheria wakopaji wasio waaminifu
- Kuweka utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Hisa na mikopo ila kwa masharti kwamba taratibu hizo zisikiuke sheria na kanuni za kikundi hiki na mfumo wa VICOBA.
- Kusimamia matumizi yote ya kikundi
- Kuandika na kutunza mihtasari ya majadiliano na maazimio yote ya mikutano ya kikundi

- Kufanya kazi nyingine zozote kama zitakavyo amriwa na wanachama wa kikundi.

19. TARATIBU ZA UTOAJI MIKOPO

Maombi yote ya mikopo yataidhinishwa na wanachama wa kikundi kizima na baada ya kukaguliwa na wanachama wa kikundi kidogo cha watu watano.

A. Mikopo ya Hisa

- Mikopo ya maendeleo italipwa katika kipindi kisichozidi miezi 3 kwa mkopo wa kwanza na miezi 6 kwa mkopo wa pili na kuendelea. Hata hivyo mkopo ambao hautazidi shilingi laki tisa utatakiwa urejeshwe ndani ya muda wa miezi sita.
- Fomu maalum ya mchanganuo wa biashara ya mwanachama itajazwa ambayo itachanganua ni jinsi gani atatumia mkopo kwa ajili ya biashara husika.
- Wanachama wote wataafiki maombi ya mkopaji na kutoa ruhusa kwa kamati ya utendaji kumkabidhi mkopaji fedha mbele ya wanachama wote.
- Mwombaji lazima azingatie kuwa hatoruhusiwa kukopa zaidi ya mara tatu ya hisa zake lakini ataruhusiwa kukopa pungufu ya mara tatu ya hisa zake na hii itategemea sana uwepo wa fedha katika kikundi na mchanganuo wa biashara yake.
- Mkopaji atatakiwa kutoa marejesho kila mwishoni mwa mwezi na kuwawezesha wengine kukopa na Yule ambaye atashindwa kurejesha atatozwa asilimia 5 ya rejesho kama faini. Lakini ikitokea mwanachama anataka kutoa marejesho kila wiki ataruhusiwa pia.
- Atakayejaza na kuwasilisha fomu ya mkopo mapema kwenye kikundi ndiye atakayepewa kipaumbele.
- Urejeshwaji wa Mikopo utafanyika kupitia M-koba.
- Mkopo utatozwa ziada ya 5% kwa muda wa miezi mitatu 10% kwa muda wa miezi sita na 15% kwa muda wa mwaka.
- Mwombaji pia atatakiwa kujaza fomu ya udhamini ambayo itatiwa saini na wajumbe watano wa kikundi kidogo (loan agreement form)
- Kama kikundi kimepata fedha kwa ajili ya kuwakopesha wanachama wake kutoka sehemu nyingine nje ya fedha za wanachama basi kitakopesha fedha hizo kulingana na kanuni itakayopendekezwa na wanachama wote wa kikundi

B. Mkopo wa Matatizo ya jamii

- Mwanachama ataruhusiwa kukopa mfuko huu kutokana na matatizo ya jamii kama yalivyo orodheshwa katika kipengele cha 16. Mkopo huu utarejeshwa kwa muda wa miezi mitatu na hautakuwa na ziada ya mkopo.

- Kiasi cha mkopo ambacho mwanachama ataruhusiwa kukopeshwa ndani ya kikundi kitatokana na kiwango chake cha mchango wa hisa na mfuko wa jamii.
- Mwanachama iwapo atakuwa amekopa mfuko mmojawapo katika matatizo ya jamii basi hataruhusiwa kukopa mwingine hadi amalize deni la kwanza lakini ataruhusiwa kukopa mfuko wa kuendeshea Biashara (mfuko wa Hisa).
- Mwanachama atakaye shindwa kurejesha fedha hizo kwa muda wa miezi mitatu hisa zake zitakatwa ili kufidia deni hilo.

20. MKUTANO MKUU WA KIKUNDI

Mwaka wa fedha wa kikundi unaishia 30/9 na mambo yafuatayo yatafanyika katika mkutano huo:-

- Kugawana faida za kikundi. Faida itakayopatikana kutokana na ziada ya mikopo mwishoni mwa mwaka itagawanywa kwa wanachama kutokana na idadi ya hisa zao.
- Kulipa madeni yote kabla ya kugawana faida
- Kukubaliana juu ya thamani ya hisa kwa ajili ya mwaka mpya wa fedha.
- Kuchagua viongozi wapya kwa ajili ya mwaka mpya wa fedha wa kikundi (Mwenyekiti, Katibu, Mweka hazina na wahesabu fedha na washika funguo)
- Mweka hazina atatoa hesabu yote ya mwaka na faida iliyopatikana.
- Kumbukumbu zote za fedha zitakaguliwa na kutolewa maamuzi na wanakikundi wenyewe.
- Kutathmini maendeleo ya kikundi.
- Kujaza nafasi zilizoachwa wazi na wanakikundi kupongenzana kwa kufanya tafrija fupi.
- Kupanga mpango mpya wa mwaka husika.

21. MAKOSA YATAKAYOTOZWA FAINI

- Mwanachama atakaye chelewa kufika kwenye mkutano wa kikundi kama ilivyokubaliwa na wanachama wote bila taarifa atatozwa faini ya Tshs 2000.
- Mwanachama atakayekosa kuhudhuria mkutano bila taarifa yoyote kwenye kikundi atatozwa faini ya Tshs 5000.
- Mwanachama atatakiwa kuwasilisha hisa zake iwapo atakuwa na sababu maalumu ya kutohudhuria kikao.

22. MENGINEYO

- Mwanachama atakaye ugua na kushindwa kufika katika mikutano atatakiwa kuendelea kufikisha michango yake ya hisa pamoja na jamii na pindi atakaposhindwa kufikisha michango atarudishiwa hisa zake na nafasi yake itaachwa wazi hadi mwishoni mwa mzunguko wa kikundi. kama hali yake itarudi kuwa nzuri na atapenda kujiunga tena basi mwanachama huyu ataruhusiwa.
- Mwanachama atakaye fariki dunia, akijiondoa au kufukuzwa uanachama katika kikundi hiki atapewa mafao yake ndani ya siku tisini
- Mwanachama yeyote atakayefiwa na baba, mama, mume, mke na watoto/tegemezi wake atachangiwa na kila mwanachama wa kikundi kuanzia shilingi 5000.
- Kikundi kitakuwa kinakutana kila mwisho wa mwezi moja Siku ambayo mshahara umeshalipwa. Kuanzia saa 11:30 jioni mpaka saa 12:30 jioni katika eneo la kazi la Mobisol (Conference room kama itakuwa ipo wazi)
- Mwanachama akifariki dunia atachangiwa kuanzia shilingi 10,000 na kila mwanachama, Ambazo atakabidhiwa mirithi wake pamoja na mafao mengine.

23. VYANZO VYA MAPATO YA KIKUNDI

- Faini
- Ruzuku
- Ziada ya mikopo
- Na mikopo kutoka katika taasisi za fedha
- Mfuko wa Hisa.